

# Pambazuko

Toleo Namba 0035

Jumatatu Aprili 24-30, 2023

**Mkono: Mwanasheria aliyeamini Biblia**

**Uk.8**

## Mayele ni mtu na nusu



**Korti yaamuru  
jogoo mkorofi  
kuchinjwa...Uk. 9**



## **Ukiondoa vyeti, kichwa chako kinabaki na nini?**

**Uk.  
5**

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

## Tahariri

**Wakati wa Katiba mpya ni sasa**

**I**JUMAA ya Oktoba 21, mwaka jana - 2022, Rais Samia Suluhu Hassan, alipokea ripoti ya Kikosi Kazi alichokiunda ili kukusanya maoni na mapendekezo kutoka kwa wananchi kwa lengo kuu moja; kuiweka Tanzania salama na bora zaidi kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Kikosi hicho kilichokuwa na wajumbe kutoka kada mbalimbali, kiliongozwa na mwenyekiti wake, Profesa Rwekaza Mukandara, ambaye ni mbobezi katika siasa na demokrasia, kilijumuisha pia wajumbe kutoka maeneo mbalimbali ikiwemo wanasiasa, asasi za kiraia, na makundi mengine, kilizunguka nchi nzima kusikiliza matamano ya Watanania kuhusu hatma ya nchi yao.

Katika mapendekezo yaliyokusanywa, ripoti iligusia masuala mbalimbali, kuanzia usawa wa jinsia, demokrasia, muundo wa Tanganyika na Zanzibar, suala la katiba mpya na zaidi sana kufunguliwa kwa milango ya fursa kwa Watanania wengi zaidi.

Ripoti hiyo, kimsingi, imejaa mapendekezo kutoka kwa wananchi waliohojiwa kueleza nchi wanayoitaka.

Hata hivyo, suala la Katiba mpya lilichukua nafasi kubwa, huku wengi waliohojiwa wakitamani kuona kunakuwepo kamati maalum ya kupitia kile kilichokusanywa kutoka kwa wananchi - wakati wa mchakato wa kupata katiba mpya.

Wanapendekeza kwamba Rasimu ya Katiba ya Jaji Warioba na Katiba Inayopendekezwa, vikusanywe na kuchambuliwa upya na wataalamu wa sheria na maeneo mengine wanaoaminika

kwa jamii ili watoe majumuisho yanayobeba mawazo ya wananchi.

Pamoja na kwamba wapo baadhi waliopendekeza kuanza upya kwa mchakato wa kupata katiba mpya, sisi katika Pambazuko tunaona ni vyema na haki kwenda na idadi kubwa ambao wanapendekeza kupitiwa upya yaliyofanywa na Tume ya Jaji Warioba.

Uhakika tulionao ni kwamba kuanza upya kwa mchakato kutaigharimu nchi fedha nyingi mno na pia muda, wakati mapendekezo ya wananchi yapo, hivyo hakuna haja ya kurejea kile kilichofanywa.

Ikiwa hayo yataridhiwa, Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kufanya hivyo, kwani Afrika Kusini mwaka 1992 ilishindwa kupata katiba mpya kutokana na mvutano wa makundi, hasa wanasiasa na ndipo iliamuriwa kuwepo kwa katiba ya mpito, huku kamati maalum ya wataalamu ikiundwa na hatimaye ikaja na katiba inayoelezwa kuwa bora zaidi Afrika.

Mbali na Afrika Kusini, majirani zetu - Kenya, mwaka 2005, serikali iliyoanzisha kura ya maoni kuhusu namna bora ya kuendesha nchi, ilishindwa kura ya maoni na kuridhia kamati maalum kupitia yale yaliyokusanywa na kupatikana kwa katiba inayotumika sasa, ikiwa imesheheni mazingira ya demokrasia pana, hata kama bado inabeba upungufu ambao unaweza kurekebishika.

Hivyo basi, ni vyema tukaamua kuwa na kamati maalum itakayopitia yaliyokusanywa na kuchakatwa na Tume ya Jaji Warioba ili kuwa na katiba mpya yenye kuondosha chembe za ukakasi katika masuala mbalimbali.

## **SICHAGULIWI MARAFIKI...**



*Mbwa akijifariji kwa marafiki zake. Anaonekana kuwa na furaha zaidi akiwa na wanyama wasiokuwa jamii yake. Ni somo kubwa kwa binadamu, kwamba wanaonekana adui mbele ya wengine, wanaweza kuwa marafiki wakubwa. (Picha imetolewa kwenye mitandao ya kijamii, mpigapicha hakujulikana).*

### **Jisajili kupata Pambazuko bure**

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

### **NUKUU**



**KUNA njia moja tu ya kuepuka kukosolewa, ukiona usiseme kitu, ukisema usiandike kitu, usifanye kitu na wala usiwe chochote. Hapo utaweza kuepuka lawama pia na kutokwaza wengine - Aristotle, Mwanafalsafa wa Ugiriki**

## Tafakuri

## Ukiondoa vyeti, kichwa chako kinabaki na nini?

Na Daniel CHONGOLO

**M**WANAFALSAFA anayehishimika zaidi duniani – mzaliwa wa Ujerumani, Albert Einstein aliwahi kuulizwa akili ni nini? Akajibu; “akili ni kile kinachobakia baada ya kuondoa yote uliyofundishwa darasani.”

Maana ya mwanazuoni huyo ni kwamba wapo watu wakiondoa yale waliyofundishwa darasani, vichwa vyao vinabaki tupu. Hawana kitu wanachokijua wala kuweza kukidadauwa.

Anasema kitu pekee walichojaza vichwani ni yale waliyofundishwa darasani na kwamba wengi wao – kwa kuhofia kubainika kwamba “hawana lolote kichwani,” hukimbilia kujisifia kuwa na vyeti vingi; ikiwamo kutaja mara kwa mara idadi ya ‘digrii’ walizonazo.

Hawa ni kwamba hawana akili ya kuhoji, kujadili wala kuchanganua mambo. Siyo wavumbuzi. Ni watu wasiokuwa na akili, ingawa wana elimu ya darasani.

Einstein anasema hakuna uhusiano kati ya elimu na akili. Maana yake ni kwamba kuna watu wana elimu, lakini hawana akili, na wengine wana akili, lakini hawana elimu. Ni bora uwe na akili ukose elimu, kuliko uwe na elimu ukose akili.

Wanazuoni wengine wa kale, wakiwamo Isaac Newton, Galileo Galilei na Archimedes wa Syracuse, hawakuwa na elimu yoyote iliyopata vyeti; iwe astashahada (cheti), stashahada (diploma) wala shahada (digrii), lakini walikuwa na akili ambazo leo wanatambulika na kurejewa kila uchao; iwe vyuoni, ofisini na hata katika ugunduzi wa kisasa katika sekta mbalimbali. Hawa ni miongoni mwa wanafalsafa wa kale wanaoiongoza dunia hadi sasa.

Akili siku zote ni “bingwa” kuliko elimu – hasa ya darasani kwa sababu akili ndio ilibuni elimu. Yaani watu wenye akili walikaa wakakubaliana waanzishe utaratibu ambao utamuwezesha mtu kukaa darasani na kujifunza kwa kipindi fulani, kisha apimwe kwa mitihani na atunukiwe cheti.

Ubunifu huo ulifanywa na wenye akili. Jiulize mtu wa kwanza kutunukiwa digrii duniani alifundishwa na nani?

Ileweke kuwa mtu mwenye akili, lakini akakosa elimu, ni msaada kwa jamii kuliko mtu mwenye elimu, lakini akakosa akili.

Tajiri na kijana wa Marekani aliyeacha elimu ya darasani, Mark Zuckerberg (miaka 39) leo anaongoza mfumo mzima wa mawasiliano ya dunia kwa kuwa alikuwa na (bado anazo) akili.

Huyu ni miongoni mwa watu waliobuni mfumo wa mawasiliano ya intaneti na njia rahisi za kuwasiliana bila kujali mipaka ya nchi wala umbali. Hivi sasa dunia inafaidi akili zake na wala siyo elimu.

Zuckerberg ndiye mmiliki wa mitandao ya kijamii ya Facebook, Whatsapp na Instagram.

Akiwa darasani wapo baadhi ya walimu wake, hasa maprofa waliomuona “kilaza” darasani, leo wanatumia ubunifu wake kuendesha maisha yao. Kama siyo Facebook, basi wanatumia Instagram au Whatsapp. Maprofa wenye elimu kubwa wamezidiwa ujanja na “kilaza” mwenye akili.

Jiulize, ukiondoa yale uliyofundishwa darasani unabaki na nini? Yaani ukiondoa hivyo vyeti ulivyopata darasani, kichwa chako kinabaki na nini?

Kama kuna kitu kinabakia basi hicho kinachobakia kinaitwa akili.

**Mwandishi ni Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).**

## **CRDB yajipanga kulea ubunifu**

**Na Scovya MANASE**

**B**ENKI ya CRDB imeazimia kutumia sehemu ya faida zake kwa kurejesha kwa jamii ili kuweka mazingira yenye kuzalisha kipato kwa idadi kubwa ya watu.

Katika mpango wake kamambe, benki hiyo inayoamini katika kukuza vipaji; hasa ubunifu wa sayansi na teknolojia, biashara na mifumo ya mawasiliano, imedhamiria kuwekeza fedha kwa vijana na wanawake, mamkundi ambayo yanatajwa kuwa msingi wa maendeleo makubwa na yenye kasi.

Benki kutekeleza hilo, CRDB imeweka mikakati kupitia programu yake mpya – iitwayo iMBEJU, ambayo itasimamiwa na kampuni yake tanzu ya CRDB Bank Foundation.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela anaeleza kuwa benki hiyo imegundua uwezo mkubwa wa vijana na wanawake wa Tanzania katika kufanya kazi za kibunifu, lakini wanakosa mafunzo na kitaji, hivyo wameamua kuwekeza huko kwa lengo kubwa la kusaidia nchi kupiga vita umasikini.

“Vijana wetu; wa kike na kiume, wanaweza mambo mengi zaidi ya kibunifu, wanakwama kwenye mitaji na wengine kushindwa kuwa na sifa za kuifikia mitaji kutoka kwenye taasisi za fedha, sasa sisi tunakuja kuweka nguvu zetu kusaidia,” amesema mtendaji huyo mkuu wa CRDB.

Inaelezwa kuwa programu yake ya iMBEJU itahakikisha kiasi cha Sh. bilioni 5 kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano, zinaingizwa ili kuhuishia mawazo bunifu, kusaidia mafunzo na hata mitaji.

“Kiasi hicho cha fedha katika programu hiyo kitakuwa endelevu kwa kuwalenga wajasiriamali wachanga, vijana wenye ubunifu mbalimbali na wanawake wenye biashara zenye bunifu kupitia ushauri, mafunzo, na ufadhili wa mitaji wezeshi,” amesema Nsekela.

Imeelezwa kuwa programu ya iMBEJU inaendeshwa kwa miundo miwili;



**Abdulmajid Nsekela**

muundo shindani wa uwezeshaji wa biashara changa za vijana, na muundo wa uwezeshaji wanawake wajasiriamali.

Tully Esther Mwambapa, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation anasema kuwa upande wa muundo shindani wa uwezeshaji wa biashara changa unafanywa kwa ushirika na serikali kupitia Tume ya Tehama na Tume ya Sayansi na Teknolojia (Costech).

Inaelezwa kuwa wenye nia ya kunufaika kupitia programu hiyo, watatakiwa kuwasilisha maombi yao kwa njia mbili; moja kwa kupitia mtandao, hasa kwa wenye mawazo bunifu na pia katika matawi ya Benki ya CRDB yanayopatikana nchi nzima.

Kinachotakiwa ni kuhakikisha kuwa mwombaji lazima awe mwanachama wa vikundi ambavyo vimeingia katika mkataba wa makubaliano ya iMBEJU na Benki ya CRDB, lengo likiwa ni kuhakikisha uendelevu wa programu na kwamba inakuwa na mwelekeo wa kunufaisha watu wengi zaidi.

## Habari

## Waandishi kufunzwa kutangaza utalii

Na Mwandishi WETU

**W**AANDISHI wa habari walioboea kutumia mifumo ya kidigiti Tanzania, watapewa mafunzo ya namna nzuri ya kuutangaza utalii wa nchi hiyo kupitia mitandao ya kijamii.

Mafunzo yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi na Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari Tanzania, Tampa, yanaelezwa kuwa na lengo kubwa la kuwapa mafunzo waandishi hao kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania kwa dunia.

Mkuu wa Utawala na Uhusiano wa Tampa, Tryruckia Mfinanga jana ameliambia Pambazuko kwamba mafunzo hayo yatafanyika Dar es Salaam na kwamba wamealika waandishi wa Dar es Salaam kwanza, ingawa lengo ni kwenda nchi nzima.

“Nchi yetu ina vivutio vingi mno, na hakika tungepaswa kuongoza kwa idadi kubwa ya watalii, lakini tuna mkwamo mahali, hasa kwenye kujitangaza, ndiyo maana utaona nchi za Kenya na Rwanda, zinajitangaza zaidi na wanapata watalii wengi...”

... Sasa na sisi Tampa tukaona ni vyema kusaidia kazi ya kuutangaza utalii wetu – kama anavyojitahidi Rais Samia Suluhu Hassani ili kutambulika zaidi, kuongeza idadi ambayo tafsiri yake, ni kuongezeka kwa kodi ikiwa wageni watakuja kwa wingi,” amesema Tryruckia.

Waandishi hao watapewa mafunzo haya; matumizi ya mitandao ya kijamii ‘kupaisha’ utalii wa Tanzania, mbinu za kufikia idadi kubwa ya wataai; na umuhimu wa teknolojia ya habari katika soko la utalii.

Tryruckia amesema kuwa mafunzo hayo ya siku moja, yatasambaa kwa mikoa mingine kadri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu na kwamba anaomba taasisi na kampuni za utalii kusaidia kusambaza elimu hiyo kupitia mafunzo



Tryruckia

yanayoratibiwa na Tampa.

Amesema kuwa mafunzo hayo yatawafikia waandishi kutoka kwa walimu wabobezi wa masuala ya utalii ambao ni wakufunzi wa Chuo cha Taifa cha Utalii, kilichopo Dar es Salaam pamoja na wataalamu wa masuala ya teknolojia ya habari.

“Lengo letu ni kuwa na waandishi wa mitandao ya kijamii, kutumia majukwaa yao kuwafikia watu wengi zaidi, hasa walioko nje ya Tanzania, ambao imebainika wengi hawasubiri kusoma magazeti wala vipeperushi, bali kupitia mitandao ya kijamii zaidi; ikiwamo Facebook, Twitter, Instagram na hata Tik Tok kwa sasa,” ameeleza Tryruckia.

Mafunzo hayo yamefadhiliwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), gazeti la kidigiti la Pambazuko na Bodi ya Utalii (TTB).



**TANZANIA**  
TOURIST BOARD

## **Raila amburuta IGP The Hague**

Na Mwandishi WETU

**D**ALILI kwamba Kenya bado hakujatulia zinaendelea kudhihiri baada ya kiongozi wa upinzani nchini humo, Raila Odinga kuomba Mahakama ya Kimataifa kuhusu Uhalifu (ICC), iliyoko The Hague, Uholanzi, kuchunguza tuhuma ilizowasilisha dhidi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi Kenya (IGP), Japhet Koome.

Raila na wafuasi wake wanadai kwamba IGP Koome amehusika moja kwa moja kutesa, kuua na kudhulumu haki za raia wa Kenya waliokuwa wakiandamana kihalali na kuruhusiwa na katiba ya nchi hiyo.

Taarifa zilizilifikia Pambazuko mwishoni mwa wiki, zinaeleza kwamba ICC bado haijajibu barua ya Raila, ingawa imekiri kupokea barua yao na kwamba “madai yao yatafanyiwa kazi mapema.”

Kiongozi Mkuu wa Mashtaka (OTP) wa mahakama hiyo, Karim Khan amesema kwamba ofisi yake imepokea barua iliyowasilishwa na Umoja wa Azimio Kenya, Alhamisi ya wiki iliyopita; Aprili 20.

Barua hiyo iliyoandikwa na Wakili Paul Mwangi inaeleza kuorodhesha majina ya Wakenya wanaodaiwa kuuawa na kuteswa; wakiwemo waaandishi wa habari na afisa mmoja wa Polisi, ambao inadaiwa waliuawa katika mashambulizi dhidi ya waandamanaji katika miji ya Nairobi na Kisumu.

Azimio, ikiongozwa na Raila, ilishindwa katika uchaguzi uliofanyika mwaka Agosti, mwaka jana na kundi la Kenya Kwanza, linaloongozwa na William Ruto. Ruto alishinda nafasi ya urais ambao unapingwa na Raila.

Baada ya kushindwa, Azimio ilianza purukushani za kutoitambua serikali ya Ruto na kuitisha maandamano nchi nzima kila wiki ili kushinikiza serikali “kuachia ngazi.”

ICC ina vigezo vyake katika kufikia hatua ya kuanza uchunguzi dhidi ya mtu yeyote, bila kujali dhamana yake, wala



**Raila**

mipaka ya nchi.

Kipengele cha 15 cha Mkataba wa Roma, ulioanzisha ICC, kinazuia kusambaza maelezo kuhusu malalamishi yaliyowasilishwa mbele yake hadi kuanza kwa mchakato wa uchunguzi.

Chini ya kipengele cha 15 cha Mkataba wa Roma, mtu yeyote au kundi la watu wanaweza kutuma taarifa, kuhusu madai ya kutendewa uhalifu, kwa kiongozi wa mashtaka ambaye ana wajibu wa kulinda usiri wa taarifa alizopokea.

Kulingana na Kipengele cha 15 cha Mkataba wa Roma, kiongozi wa mashtaka anaweza kushughulikia taarifa kama hiyo “achambue uzito wa taarifa aliyopokea na anaweza kuomba maelezo zaidi kutoka nchi mwanachama, asasi za Umoja wa Mataifa au mashirika ya serikali au yale yasiyo ya kiserikali”.

Endapo kiongozi wa mashtaka atagundua kuwa “kuna sababu ya kuanzishwa kwa uchunguzi, ofisi hiyo itawasilisha ombi kwa majaji wa ICC ili ipewe kibali cha kuanzisha uchunguzi.

Ikiwa majaji, baada ya kuchunguza ombi hilo na ushahidi uliotolewa, kuna sababu ya uchunguzi kuanzishwa na kesi hiyo ni miongoni mwa zile hushughulikiwa na mahakama hiyo, wataidhinisha uchunguzi uanzishwe,” inasema sehemu ya nne ya kipengele hicho.

## Buriani

## Mkono: Mwanasheria aliyeamini Biblia zaidi

Na Derek MURUSURI

**N**ILIALIKWA nyumbani kwa wakili Nimrod Elirehema Mkono kwa ajili ya mazungumzo, tukiwa nyumbani kwake, Dar es Salaam, sikuamini kusikia; “karibu chumbani kwangu.”

Sikuamini kwa kuwa siyo kawaida “mtu mkubwa, msomi na tajiri” kukuingiza chumbani kwake anapolala.

Aliniambia, “usiwe na wasiwasi, wala hofu, nakukaribisha chumbani ili kufuata kitu ambacho hakiwezi kutoka huko kwenda popote. Hubaki humohumo miaka yote na hakiwezi hata kushuka huko chini.”

Kumbe huko chumbani kwake – ghorofani, tulifuata Biblia.

Hapo nikajifunza kitu; kwamba pamoja na utajiri wake wote, alikuwa mcha Mungu.

Akanifungulia Maandiko Matakatiifu, mistari inayoeleza mambo ya mfalme aliyekuwa shujaa, Nimrod; wajina wake.

Nimrod wa kwenye Biblia anaeleza kwa alikuwa mtoto wa Kushi, mjukuu wa Ham na kitukuu cha Nuhu; yule aliyejenga safina.

Baada ya kumaliza kusoma Biblia, tukashuka na kwenda kupanda gari lake - Vogue, tukaenda kukagua ujenzi wa maabara aliyokuwa anajenga katika Shule ya Msingi Oysterbay, jijini Dar es Salaam.

Baada ya ukaguzi huo, ndipo tukaendesha gari kwenda Ukumbi wa Karimjee. Sijui alitaka kunifundisha nini.

Akaniuliza, kwanini unadhani Karimjee ameandikwa hapa na alifanya nini?

Nikamjibu; “ninafahamu kuwa ndiye aliyetoa jengo hili kutumika kama Baraza la Kutunga Sheria na baadaye Bunge la Tanganyika,” akasema umejibu vizuri.

Wakili Nimrod Elirehema Mkono akanieleza mengi kuhusu kuacha alama na kutumikia nchi na watu wake kwa moyo, akasema yeye anaamini katika



**Nimrod Mkono**

kusaidia, hasa watu wenye hali duni za maisha ili kuwakomboa.

Akasema, moyo wake umekuwa ukimsukuma kufanya zaidi na zaidi na wala halazimishwi na mtu, lakini kwa kuchukia ufukara, amekuwa akitenda kila analoweza kukwamua mtu mmoja mmoja, familia na hata taifa.

Kauli hii ya Wakili Mkono, inasadifu mengi makubwa alifanya kwa jamii yake; tena siyo eneo alikozaliwa tu – Mkoa wa Mara, bali maeneo mengi nchini.

Habari za kifo chake, hakika zimestua wengi kutokana na namna aliyowagusa kwa kuhakikisha mali alizokuwa nazo, zinasaidia kukwamua maisha mabovu ya watu.

Mkono kwa fedha zake amejenga shule za msingi na sekondari ambazo ni pamoja na Chifu Ihunyo, Chifu Wanzagi, Chifu Oswald Mang’ombe, Butuguri na Kasoma zilizoko Mara na Shule ya Msingi Busegwe. Alikuwa Mbunge wa Musoma Vijijini.

Aidha, Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Julius Nyerere (MJNUAT), yeye Mkono ndiye muasisi wake.

Mkono alifariki dunia alifajiri ya Aprili 18, 2023, akiwa nchini Marekani.



## **Korti yaamuru jogoo mkorofi kuchinjwa**

**Na Mwandishi WETU,**

**I**NAWEZA kuelezwa kuwa ni kituko cha mwaka, lakini ndiyo ukweli na nguvu ya mahakama – kwamba hukumu yake hutekelezwa mara moja, labda uwepo upande unaopinga na kukata rufaa.

Jumatatu iliyopita - Agosti 17 itabaki kwenye kumbukumbu za mahakama, mawakili, wananchi kwamba siku hiyo mahakama iliamuru kuchinjwa kwa jogoo lililobainika pasi na shaka kwamba lilikuwa linakiuka sheria na kuvunja haki za watu.

Kosa la jogoo hilo ni kuendelea kuwika muda mrefu, hata kabla ya kukucha.

Kwamba mahakama iliridhika kwamba jogoo hilo lilikuwa likiwanayima usingizi majirani zake na kuwakosesha haki ao ya kupumzika.

Hakimu wa Mahakama ya Mji wa Kano, Nigeria, aliamuru jogoo huyo kuchinjwa licha ya mawakili wa upande wa utetezi na mwenye jogoo huyo kuomba mahakama hiyo iamue tofauti.

Pamoja na hukumu huyo, hakimu hakueleza nyama ya jogoo huyo ifanywe nini; kwamba aliacha suala hilo mikononi mwa mwenye jogoo.

Hakimu mkuu wa mahakama hiyo, Halima Wali, alitoa hukumu hiyo baada ya majirani wawili kuwasilisha shauri mbele yake wakilalamika kuwa jogoo huwakosesha usingizi kwa kuwika “usiku kucha, haswa alfajiri ambapo usingizi huwa mnono zaidi.”

Mbali na kuwika mara kwa mara, jogoo huyo alituhimiwa kwa kutembea kwa kishindo, kiasi cha kuwatia hofu majirani zake. Kwamba majirani walikuwa wakikosa amani kusikia “kishindo” kinachokaribia cha binadamu wanapokuwa wamepumzika.

Mmoja wa walalamishi hao, Yusuf Mohammed, mwenye makazi yake eneo la Ja'en – jirani na nyumba anamoishi jogoo huyo, alieleza mahakama hiyo kwamba kuwika kwa jogoo huyo kila mara “kunampokonya haki yake ya msingi ya kulala.”



**Jogoo**

Mwenye jogoo hilo, alikiri tuhuma zote zilizowasilishwa na upande wa mashitaka, lakini akijitetea kwamba huyo ni kiumbe wa Mungu ambaye hajui endapo anawanyima binadamu haki zao za msingi.

“Mheshimiwa hakimu, jogoo huyo ni kiumbe wa Mwenyezi Mungu, hawa majirani zangu wanasumbuliwa na shida nyingine, na wala siyo kuku (jogoo) wangu,” alisema Isyaky Shu'aibu, huku akiungwa mkono na wakili wake.

Mawakili wake waliomba hukumu hiyo kusitishwa, huku wakieleza kwamba mteja wao amekubali kumfungia jogoo huyo kwenye banda ambalo halitakuwa chanzo cha kelele.

Wakili upande wa mashitaka alihoji; “je, akiwa ndani ya banda hilo, hatawika na kuleta usumbufu uleule unaopiganiwa mahakamani hapo?” Upande wa utetezi haukuwa na jibu lililoiridhisha mahakama, hivyo hukumu kutaka utekelezaji.

Hukumu hiyo ilitekelezwa juzi – Ijumaa kwa jogoo huyo kuchinjwa, ingawa haikufahamika mara moja wapi na nani alichukua nyama kwenda kufanya kitoweo.

**Imetafsiriwa kutoka kwenye vyombo vya habari vya Nigeria**

**Habari****Mayele ageuka mtu na nusu****Na Juma MABRUK**

**M**SHAMBULIAJI mahiri wa Timu ya Yanga ya Tanzania, Fiston Mayele, jana aliwezesha klabu yake kuanza vyema michuano ya kuwania ubingwa wa Kombe la Shirikisho Afrika, baada ya kuweka kimiani mabao mawili ndani ya dakika nane.

Yanga ikicheza mchezo wake wa robo failali dhidi ya Timu ya Rivers United ya Nigeria, iliitangaza vyema Tanzania kwa kuibuka na ushindi huo. Mabao hayo mawili yaliyofungwa na Mayele katika dakika ya 73 na baada ya kipindi kifupi cha dakika saba, akatupia bao la pili dakika ya 81.

Kelele, nderemo na vifijo vya mashabiki wachache waliokuwemo ndani ya Uwanja wa Godswill Akpabio, ulioko Jiji la Uyo, Nigeria, kabla hazijapoa, Mayele “akafanya yake” na kushangilia kwa staili ileile ya kupigapiga mikono na baadaye kutetema.

Yanga wakati wa kipindi cha kwanza walionekana kucheza kwa kulinda zaidi lango lao, mbinu ambayo iliaweka mashabiki wao roho juu, kwani walisikika wakilalamika mfumo wa uchezaji wa 5-3-2, ambao ni maarufu kwa kujilinda zaidi kuliko kushambulia.

Wachambuzi wa kabumbu wanaelezea mfumo huo kuwa wenye hatari kubwa zaidi ikiwa wapinzani wanakuwa na washambuliaji wenye kasi kubwa na nguvu za kusakama lango, hivyo kuwa na uwezekano wa kupata mabao kirahisi. Kwamba mfumo huo hutumika zaidi kwa timu ambayo inaongoza kwa kufunga na sasa inalinda lango zaidi.

Ni kutokana na mfumo huo, kipindi cha kwanza Yanga haikupata nafasi nyingi za kushambulia na wachezaji wake wa mbele, walikuwa wakikaba zaidi kuliko kusukuma mpira mbele ili kuweza kupata bao.

Hata hivyo, Yanga walionekana kubadili mfumo katika kipindi cha pili na walikuwa na kasi kubwa ya kusukuma mpira mbele kwa washambuliaji wake ambao, dakika 28 baada ya kuingia

**Mayele**

uwanjani kuanza kipindi hicho, Mayele aliweka bao la kwanza kimiani.

Bao hilo liliwavuruga wapinzani wao na wakati bado hawajakaa sawa, Mayele tena, akawachanganya zaidi kwa kufunga bao la pili.

Kufuatia ushindi huo, rekodi ya Rivers imeharibiwa na sasa Yanga inakuwa timu pili kuichapa ikiwa nyumbani kwao – Nigeria. Timu hiyo ambayo imecheza michezo 15 ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF) ikiwa nyumbani ilifungwa bao 1-0 katika mchezo wake dhidi ya Far Rabat ya Morocco. Imeshinda michezo 12 na suluhu moja.

Ikiwa Yanga itashinda ama kutoka sare – dhidi ya Rivers katika mchezo wa marudio utakaochezwa Dar es Salaam, siku sita zijazo – Aprili 30, upo uwezekano mkubwa wa kuonyeshana ubabe kwa mshindi kati ya Pyramids ya Misri au Marumo Gallants kutoka “Bondeni” - Afrika Kusini.

## Ng'wanamalundi na miujiza yenye maswali mengi - V

**Na Ibengwe Shileki MAZEGE**

**A**KIWA gerezani, Mwanamalundi aliwekwa chumba kimoja na mtemi Makongoro Igana. Mtemi Makongoro akamuuliza Mwanamalundi, “Hivi huna namna ya kujiokoa mahali hapa?” Mwanamalundi akamjibu kuwa kwa wakati huo hangeweza kujiokoa, ila kuna miujiza ya shoka na maziwa amemuachia mama yake nyumbani.

Mtemi akamuuliza, “Una miujiza mingine yoyote?” Mwanamalundi akamwambia Mtemi Makongoro kuwa anaweza kupanda viazi na mihogo na ikavunwa ndani ya dakika kadhaa tu na ikawa tayari kabisa kwa chakula.

Wakiwa kisiwani hapo, wakakubaliana kwenda ng'ambo ya kisiwa kisha wakachukue mbegu za viazi na mihogo ili washuhudie miujiza hiyo ya kupanda na kuvuna ndani ya dakika kadhaa.

Kwa kuwa nyakati hizo wafungwa wa visiwani walikuwa wakiachwa huru kwa kuwa hawataweza kutoroka, Mwanamalundi na Mtemi Makongoro walienda mpaka ufukweni mwa bahari.

Wakati huo Makongoro akiwa ameshika jiwe na Mwanamalundi akiwa ameshika fimbo. Makongoro aliporusua jiwe umbali mrefu baharini, Mwanamalundi aliyapiga maji kwa fimbo na kisha maji yakajitenga na kuacha njia mpaka pale lilipotua jiwe. Walifanya hivyo mpaka walivyofika bara na baadaye kurejea.

Ukawa mchezo wao kwenda bara, kila walipokuwa wakitoroka gerezani, waliacha vivuli vyao vilivyoonekana kama watu halisi. Kuna nyakati Mwanamalundi na Mtemi Makongoro walionekana wakiwa Mwanza au Shinyanga na gerezani pia muda huohuo. Jambo hili liliwachanganya sana Wajerumani.

Walipomaliza vifungo vyao, walirudishwa nyumbani kwao kwa ndege. Jamii ya Mwanamalundi ilipoona ndugu yao amerudishwa kwa ndege wakaamua kumpa jina jipya, “Ng'wenhwandenge”,



**Mwanamalundi**

wakimaanisha “aliyerudishwa kwa ndege.” Mwanamalundi anaaminika kuwa ndiye msukuma wa kwanza kupanda ndege.

Wakati anarudishwa nyumbani baada ya kumaliza kifungo chake, mama yake alifurahi sana kwa sababu maziwa hayakuganda kwa miaka mitatu, jambo ambalo lilionesha kuwa huko aliko alikuwa hai. Maziwa yalibaki katika ubora ulele kwa miaka mitatu.

Inaelezwa pia, shoka aliloliacha likining'nia, lilianza kuteremka taratibu kwenye ukuta kadiri Mwanamalundi alivyokuwa akikaribia kufika nyumbani. Alivyofika tu, shoka ilikuwa imefika ardhini kuashiri kuwa muda wowote Mwanamalundi atafika hapo. Na ndivyo ilivyokuwa.

Aliporudi mtaani, Mwanamalundi hakuacha asili yake. Aliendelea kucheza ngoma maeneo mbalimbali. Mtemi Masanja ambaye aliyesababisha Mwanamalundi kunusurika kunyongwa na hatimaye kufungwa, aliamua kumfukuza Mwanamalundi katika himaya ya utawala wake.

Mwanamaundi akaamua kuhamia kijiji kiitwacho Seke kwa Mtemi Mahizi ambako aliendelea kucheza ngoma na kufanya miujiza yake.

Akiwa Seke wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga; Mwanamalundi alifanya muujiza uliomoongezea heshima kijijini humo. Wanakijiji cha Seke walibiwa ng'ombe wengi na Wamasai kutoka Tabora. Wanakijiji wakataka kwenda

**Watu Maarufu****Ng'wanamalundi na miujiza  
yenye maswali mengi - V***Inatoka Uk. 11*

kufuatilia ng'ombe hao usiku huohuo, jambo ambalo Mwanamalundi alikataa.

Mwanamalundi aliwahakikishia wanakijiji kuwa ng'ombe hao wapo salama na watarudishwa salama tu kesho asubuhi na siyo usiku huo. Wanakijiji walikubali kutokana na kumuamini Mwanamalundi.

Usiku wa siku hiyo, Mwanamalundi akatuma nguvu zake zilizowazingira Wamasai na kisha kuwafanya wasinzie. Na ilipotimu asubuhi, inaelezwa kwamba, ng'ombe hao walianza kurejea wsalikoibwa.

Wanakijiji waliwafuata Wamasai wale waliokuwa wamelala na kuwaua.

Kuna kipindi, Mwanamalundi alivamia pori la Mtemi wa Ng'hung'hu aitwaye Chalya ili achimbe mizizi fulani ya dawa. Mtemi Chalya alipata "machale" kuwa kuna mvamizi katika mapori yake anachimba mizizi ya dawa.

Mtemi akaondoka na kuelekea kule ambako machale yalimuelekeza. Ni kweli, akamkuta Mwanamalundi akichimba mizizi ya dawa. Mtemi akamuuliza Mwanamalundi, "ni kwanini umeingia katika utemi wangu bila kunijulisha?" Mwanamalundi akajibu, "wewe ni mtemi wa watu wote ila mimi ndiye mtemi wa miti yote!"

Jibu hilo lilimkwaza Mtemi Chalya ambaye aliamua kurudi kwenye himaya yake kwa ghadhabu na kuwaamuru askari wake wamkamate Mwanamalundi ili aadhibiwe.

Askari wakiwa wameambatana na Mtemi Chalya walipofika porini eneo alilokuwepo Mwanamalundi, hawakumkuta. Badala yake waliwakuta simba wengi wakiwa wamelala eneo hilo. Ilibidi watimue mbio kujiokoa wenyewe dhidi ya simba hao.

Walipofika kwenye himaya ya mtemi wakiwa salama, walimkuta Mwanamalundi amemaliza kula chakula chao na anaondoka. Ilibidi mtemi

*Mmoja wa wazee wa kisukuma*

amuache tu Mwanamalundi aondoke bila kumbughudhi kwa lolote.

Mwanamalundi alifariki dunia mwaka 1936 kwa maradhi ya kawaida na kuzikwa Ididi Jihu huko kijiji cha Seke wilaya Kishapu mkoa wa Shinyanga akiwa ana umri wa miaka 44.

Tukio la kifo chake lilitwa "hang'witulo gwa shigela" ikimaanisha "vita vya kuwakimbia wamasai". Hii ni kwa sababu wakati Mwanamalundi anakata roho, kulitokea kishindo kikubwa kama tetemeko la ardhi. Watu wengi walikimbia ovyo kwa hofu kuwa labda Wamasai wamevamia eneo lao ili kuwaua.

Baada ya kishindo hicho, giza likaingia ghafla, giza ambalo hata kuku wakaanza kurudi wanakolala, fisi wakaanza kutembea mitaani wakidhani ni usiku. Hata baada ya mazishi yake, kaburi lake lilifuka moshi mwingi uliopanda mpaka juu mawinguni na kutengeneza giza la muda mfupi.

Mwanamalundi anakumbukwa pia kwa kuweza kutembea hewani bila kukanyaga ardhi, kujibadili na kuwa kiumbe tofauti kama mnyama, ndege, majani, mti au jiwe na uwezo wake wa kutembea juu ya maji au kuwa ndani ya maji kwa muda mrefu.

Mwanamalundi ni mmoja tu wa watu mashuhuri katika tawala za Kisukuma. Kuna watu mashuhuri kabla yake kama akina Nindwa, Italange na Sita. Hawa wote walikuwa ni watu wa miujiza kama alivyokuwa Mwanamalundi.

## Waafrika mamboleo na maadili asilia

Na Digna DESIRATA

**L**IPO swali muhimu juu ya majukumu **L**ya kimaadili linalouliza; “sifa zinazoambatana na hulka ya ubinadamu kuhusu matendo yapi yenye mchango chanya kwa ustawi na matendo gani yenye mchango hasi kwa ustawi,” majibu ya Waafrika mamboleo ni haya;

Kwamba, kanuni za maadili ni seti ya miongozo kuhusu matendo yanayopaswa kufanyika, au kuepukwa, kwa ajili ya kulinda tunu za kibinadamu.

Miongozo hii ikiwa inaunda mkakati wa kufanikisha ustawi wa watu kwa kutaja haki na majukumu kati ya mtu na nafsi yake, kwa upande mmoja, na haki na majukumu kati ya mtu na jamii yake, kwa upande mwingine;

Kwamba, kila haki inayofahamika inazo sehemu nne, yaani: madai kuhusu kitendo kinachopaswa kufanyika au kutofanyika, mleta madai, mdaiwa, na sababu ya madai husika; ambapo, mdaiwa anao wajibu wa kutimiza madai husika. Kuna haki za aina nne.


Katika uhusiano wa watu wawili, matendo yanayopaswa kufanywa na mtu wa kwanza kwa faida yake, bila hofu ya kuulizwa na mtu wa pili, yanaitwa haki za uhuru chanya.

Mfano wa hili ni haki ya mtu wa kwanza kuvuta sigara akiwa peke yake ukumbini, kwa kuwa hakuna kanuni inayotaja jukumu la kujizuia kuvuta sigara, jambo ambalo lingekuwa sababu ya kuhojiwa na mtu wa pili;

Katika uhusiano wa watu wawili, matendo yanayopaswa kuepukwa na mtu wa kwanza kwa faida yake, bila hofu ya kuulizwa na mtu wa pili, yanaitwa haki za uhuru hasi.

Mfano ni haki ya mtu wa kwanza kutovuta sigara, kwa kuwa hakuna kanuni inayotaja jukumu la kuvuta sigara, jambo ambalo lingekuwa sababu ya kuhojiwa na mtu wa pili;

Uhusiano wa watu wawili, matendo yanayopaswa kufanywa na mtu wa



*Tempels*

kwanza, kwa faida ya mtu wa pili, kwa kuwa kuna kanuni inataja wajibu huo, yanaitwa haki za madai chanya, mfano ni madai ya mtu wa pili kwamba mtu wa kwanza anao wajibu wa kumlipa deni lake;

Katika uhusiano wa watu wawili, matendo yanayopaswa kuepukwa na mtu wa kwanza, kwa faida ya mtu wa pili, kwa kuwa kuna kanuni inataja wajibu huo, yanaitwa haki za madai hasi, mfano ni madai ya mtu wa pili kwamba mtu wa kwanza anao wajibu wa kujizuia kuiba kalamu yake;

Kwa ujumla, haki zinazohusiana na madai chanya hutimizwa kupitia majukumu chanya (maagizo). Mfano ni jukumu linalotokana na agizo la “kuwatunza watoto, kuwasaidia yatima na kufanya kazi.”

Na haki zinazohusiana na madai hasi hutimizwa kupitia majukumu hasi (makatazo). Mfano ni jukumu linalotokana na makatazo kama vile “usiue, usiibe, usidanganye.”

Jawabu kwa swali la kimantiki Kuhusu swali la mchujo wa kimantiki linalouliza, “tunawezaje kuchuja na kupata kanuni za kimaadili kutokana na

## Uchambuzi

## Waafrika mamboleo na maadili asilia

*Inatoka Uk. 13*

maarifa yetu kuhusu sifa zinazoambatana na hulka ya ubinadamu, lakini bila kuvunja kanuni za kimantiki,” majibu ya kambi hii ni haya:

Kwamba, kanuni muhimu ya kufanya mchujo wa kimantiki kuanzia kwenye madokezo kuelekea kwenye hitimisho, inasema kuwa, taarifa zote zilizo kwenye hitimisho lazima zitokane na taarifa zilizo kwenye madokezo;

Kwamba, taarifa zinazobebwa na kanuni za kimaumbile zinaongelea hali ya mambo yaliyoyo, au hali ya mambo yanavyopaswa kuwa bila kujali kama binadamu anataka au hataki hali hiyo itokee; wakati taarifa zinazobebwa na kanuni za kimaadili zinaongelea matendo yanavyopaswa kufanywa au kutofanywa na binadamu kwa kuzingatia hiari ya kiuamuzi wa binadamu huyo;

Kwamba, kwa hiyo, taarifa za kimaadili zilizo kwenye hitimisho haziwezi kutokana na taarifa za kimaumbile pekee zilizo kwenye madokezo ya hoja husika, pasipo kuongeza angalau dokezo moja lenye taarifa za kimaadili, kusudi liwe daraka kati ya madokezo ya kimaumbile na hitimisho la kimaadili.

Hivyo, hoja ifuatayo ingekuwa batili kimantiki kama dokezo la pili, lenye kubeba taarifa za kimaadili, lisingekuwepo:

Mfano: “sumu ya hemloki inaua watu, watu wanapaswa kuhami uhai ili kuepuka kifo, hivyo watu wanapaswa kuepuka sumu ya hemloki.”

Kwamba, “nadharia ya Kiafrika kuhusu maadili asilia,” kama ilivyofafanuliwa hapa, inajumuisha fikra nzuri kutoka kwenye “ndharia kongwe ya maadili asilia” kutoka Ulaya, na inajumuisha fikra nzuri kutoka kwenye “ndharia mamboleo ya maadili asilia” kutoka Amerika.

Ni nadharia inayomruhusu mama kumnyonyesha mtoto wake kwa maziwa ya mpira pale anakuwa hana muda wa kumnyonyesha maziwa ya matiti; inaruhusu matumizi ya pafyumu za kuzua jasho; inakataza mauaji ya



Machiavelli

mtu asiye na hatia; inakataza wizi; na inakataa kanuni ya umachiaveli. Mfumo wa maadili ya Kiafrika unajitosheleza.

Majumuisho na mapendekezo

Hivyo, napendekeza kufunga makala hii kwa kutumia maneno ya Tempels (1959:73) anayesema haya:

“Ugunduzi kwamba kuna falsafa ya kiafrika ni tukio linalowakera wake wenye dhamira ya kuelimisha Afrika. Sisi wamisionari tulikuwa na fikra kwamba tulikuwa tumesimama mbele ya Waafrika kama watu wazima wanavyosimama mbele ya watoto.

“Katika utume wetu wa kuelimisha na kustaarabisha, tulihamini kwamba tunapaswa kuanza na ubongo ulio kama sahani tupu, yaani ‘tabula rasa,’ japo pia tulihamini kwamba tunapaswa kuandaa mazingira ya utume wetu kwa kusafisha fikra zao potofu, na hivyo kujenga msingi wa utume wetu kwenye udongo usio na miiba.”

“Tulikuwa tunaamini kabisa kwamba tunapaswa kusafisha mila potofu, imani potofu, kwa kuamini kuwa zilikuwa za kijinga na batili.”

“Hii ndiyo sababu sasa tunajikuta kwamba tunakanyaga udongo wenye kuteleza; kwamba, na tunapoteza dira, na kuanza kujuiliza, tufanye nini sasa ili tuweze kuwaongoza watu weusi?”

# Tangaza na Pambazuko

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.



*Kwa bei nafuu sana*

0744 768 263 au Barua-  
Pepe; [info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz)

## Imani

# Siasa ni dini katika kuleta ustawi

**Na Benedict MSOFE,  
Vatican City**

**P**ASIPOKUWEPO uchunguzi makini, ni rahisi kufikiri kuwa kazi ya wajumbe mbalimbali wa Mungu ni kuhusika tu na masuala ya kidini. Kumbé wana kazi kubwa ya kuhuisha, siyo imani tu, bali wanahusika na maisha ya kila siku ya binadamu

Katika “Agano la Kale” la Biblia kwa mfano, huonekana kazi kubwa ya makuhani katika utumishi wa hekaluni. Manabii nao hujifafanuna vyema katika kuwakumbusha watu juu ya kutoiacha sheria ya Mungu.

Lakini ukweli ni kwamba kazi ya Mungu kupitia wajumbe wake mbalimbali, hugusa nyanja zote za maisha ya mwanadamu. Hii ni kwa sababu Mungu hawakumbuki wanadamu wanapokuwa tu katika nyumba za ibada, bali anawezesha maisha yao katika nyanja zote.

Hivi pia ndivyo anavyopaswa mwanadamu kuenenda – yaani kuzifanya zile tunu za Kimungu kuwa sehemu ya muhimu ya maisha yake ya kila siku katika nyanja zote.

Baadhi ya nyanja zilizoshughulikiwa kwa ukaribu zaidi na kazi za manabii wa “Agano la Kale” ni jamii na siasa.

Mara nyingi ujumbe wa Mungu kupitia manabii uliwaonya wakuu wa taifa ama la Israeli au Yuda, juu ya mienendo yao. Maonyo haya hayakuhusu tu maisha binafsi ya wafalme (rej. Nabii Nathani kwa Daudi – 2 Samweli 12:1 - 25). Yalihusu pia uamuzi muhimu wa kiutawala kama vile namna ya uhusiano na mataifa mengine.

Nabii Isaya kwa mfano, mara kadhaa aliwaonya wafalme wa Yuda juu ya mienendo yao katika uhusiano wa kimataifa. Wakati taifa la Yuda likiwa katika kilele cha mafanikio ya kiuchumi na kujizolea sifa nyingi, polepole tangu mwaka 745 K., taifa la Assiria chini ya mfalme Tiglat – Pileser lilianza kuvamia mataifa mengine na kuyazingira.



*Kiongozi wa Kanisa Katoliki Papa Francis*

Liliwalazimisha walipe kodi kubwa. Mkono usio na huruma ungewapiga vikali wale ambao wagekataa kulipa kodi.

Mfalme Ahazi wa Yuda katika hekima yake, alikataa ushawishi wa taifa la Israeli na mengine yaliyodhamiria kuigomea Assiria.

Yuda ikatishwa na mataifa hayo ya jirani na katika hofu yake Mfalme Ahazi akataka kufanya makubaliano na Assiria (kujiweka kabisa chini ya utawala wake) ili kuwashinda majirani zake.

Awali mfalme alifanya uamuzi sahihi wa hekima kubaki mtiifu kwa Assiria, lakini alikuwa anaenda kufanya kosa kubwa kujiunga kabisa na taifa hilo.


Ujumbe wa Mwenyezi Mungu kupitia nabii Isaya ulimkataa Ahazi kufanya hivyo (rej. Isaiiah 7:3 – 9). Hofu ya uvamizi na kukosa utetezi wenye mantiki kwa wananchi wake waliokuwa wamechoshwa na kukandamizwa, vilimfanya Ahazi akatekeleza azma yake na akaisalimisha nchi yake kwa Assiria kinyume na maonyo ya Mwenyezi Mungu.

Swali la kujiuliza ni mataifa yetu leo yanachukua vipi uamuzi juu ya sera za kimataifa. Hakuna nyakati ambapo uamuzi sahihi hudhaniwa kuwa makosa na makosa kudhaniwa kuwa sahihi?

**Mwandishi ni mwanazuoni wa  
Elimu Katoliki huko Vatican.**



## Baraza la Eid



iongozi mbalimbali wa siasa, madhehebu Jumamosi iliyopita – Aprili 22, waliungana na Rais Samia Suluhu Hassan na waumini wa Dini ya Kiislamu kwenye Baraza la Eid ambalo kitaifa limefanyika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam. (Picha na Ikulu).



**Sudan****Sudan bado kwafuka moshi****Khartoum, SUDAN**

**M**ILIO ya risasi iliendelea kusikika Ijumaa jioni katika Mji Mkuu wa Sudan, Khartoum ingawa awali, wanajeshi wa vikosi vinavyopigana vilitangaza kusitisha mapigano kutoa nafasi kwa sherehe za Eid.

Wanajeshi waaminifu kwa naibu mkuu wa majeshi ya nchi hiyo, Hamda Daglo, ambaye ni kamanda wa kikosi cha Rapid Support Forces (RSF), walisema walikuwa tayari kuruhusu kufunguliwa kwa viwanja vya ndege kutoa nafasi kwa usafirishaji raia wa kigeni kutoka Sudan.

Umoja wa Mataifa (UN), Marekani, Uingereza, Japan, Uswisi, Korea Kusini, Uswidi na Hispania zimesema zinajiandaa kuondoa wafanyakazi wao nchini Sudan ili wasipatwe madhara makubwa, ikiwamo vifo katika mapigano hayo ambayo yamedumu kwa wiki moja sasa.

Zaidi ya watu 400 wameuawa na maelfu ya wengine kujeruhiwa katika vita hivyo kati ya wanajeshi watifu kwa Mkuu wa Majeshi Abdel Fattah al-Burhan na wale watifu kwa naibu wake, Jenerali Hamdan Daglo.

UN inasema machafuko Sudan yamesababisha changamoto kubwa za kibinadamu katika taifa hilo ambalo hutegemea chakula cha msaa.

Mapigano makali yaliendelea kati ya vikosi vya upinzani vya wanajeshi katika vitongoji vya wakazi wengi kati na kaskazini mwa Khartoum, mashahidi walisema, huku watu wengi wakisalia majumbani bila maji, chakula wala kuwepo kwa umeme.

Iliaminika kuwa Ijumaa iliyopita, majeshi hayo yanayopigania kuunda serikali, yangesitisha mapigano, lakini hakuna kilichotekelezwa na milio ya risasi na mabomu iliendelea kusikika.

Majeshi hayo, yanaonekana kukaidi kuheshimu mwito wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres na Waziri wa Mambo ya Nje wa



**Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres**

Marekani, Antony Blinken ya kusitisha vita “angalau kwa siku tatu kutoa nafasi kwa sherehe za Sikukuu ya Eid ul-Fitr.

Blinken alisema viongozi wa kijeshi na wale wa makundi ya kiraia sharti waanzishe mazungumzo ya kurejesha amani Sudan ili kuzuia kusambaratika kwa nchi hiyo.

Viongozi wa majeshi hayo wamekuwa na tofauti kubwa kuhusu nani awe kiongozi wa nchi hiyo, kati ya kiongozi wa sasa na msaidizi wake.

Jeshi la Marekani jana lilifanikiwa kuwaokoa wanadiplomasia wa nchi hiyo na familia zao kutoka Khartoum, Rais Joe Biden amesema.

“Leo (jana), kwa agizo langu, jeshi la Marekani limefanya operesheni ya kuwaondoa wafanyakazi wa Serikali ya Marekani mjini Khartoum,” alisema katika taarifa yake.

Mapema kikosi cha kijeshi cha Sudan Rapid Support Forces (RSF) kilisema kuwa ndege sita za kijeshi zilitumiwa jana katika operesheni ya mapema asubuhi, na kwamba kiliratibu uokoaji huo pamoja na Marekani.



### Na Mashala MALEZU

**M**CHEZO wa kimatafa wa masumbwi kati ya bondia kutoka Tanzania, Twaha 'Kiduku' Kassim na mpinzani wake, Iago Kiziria raia wa Georia, uliofanyika juzi; Jumamosi – Aprili 22, mjini Morogoro, umedhihirisha namna mabondia wengi wa Tanzania wanahitaji mazoezi zaidi.

Staili ya mchezo wa Kiduku unahitaji kurekebishwa ama kuachwa kabisa katika ulimwengu wa masumbwi ya kisasa, ambapo nguvu na kasi hutumika zaidi kushinda pambano.

Kiduku, pamoja na kwamba ni bingwa wa kutumia mikono na mabega yake kujilinda, lakini akikutana na bondia anayepigana kwa kasi na kusukuma “panchi” za nguvu, nafasi yake ya kushindi inakuwa finyu.

“Pamoja na kwamba Kiduku alishinda kwa pointi pambano la juzi, anahitaji kuwa mbunifu zaidi na kujenga pumzi ya kutosha zaidi, ili kupata muda mrefu wa kuhimili raundi nyingi zaidi,” amesema Kibole Mashauri, mwalimu wa ngumi

katika gym ya Kilezo, Bunju, Dar es Salaam.

Mwalimu huyo amesema kama mpinzani wa Kiduku angekuwa na ngumu nzito zaidi, angemondosha Mtanzania huyo katika raundi kuanzia ya nane na tisa.

Kwamba katika raundi hizo, Kiduku aliponekana kuchoka na alikuwa akipiga ngumi zisizokuwa na nguvu na kwamba alionekana “kukata pumzi.”

Ushindi wa pointi wa Kiduku, ulimfanya kutangazwa kuwa bingwa wa mabara wa UBO na PST baada ya kumaliza raundi zote 10.

Mpinzani wa Kiduku, raia wa Georgia, alionyesha umahiri mkubwa kumkabili Kiduku katika raundi za sita, saba na kuendelea hadi ya 10, mchezo ulipomalizika.

Kushindwa “kuumlambisha sakafu” mpinzani wake, Kiziria anabaki kuwa na rekodi ya kutoshindwa kwa kwa ‘knockout – KO, tangu kuanza kupanda ulingoni.

Ushindi wa Kiduku ulipatikana baada ya majaji wawili kumpa ushindi wa uwiano wa pointi 98-92 na 97-93.

## **BAHATISHA MAELEZO NA USHINDE – 10,000/-**

*Yeyote anaweza kuandika maelezo ya picha hii atakavyo. Wapo wanaoweza kuipa maneno kwamba - furaha ya mwana baada ya kuwa na uhakika wa chakula cha leo na siku inayofuata; wapo pia wanaoweza kudai, kijana anafurahia wazazi wake kutimiza majukumu yao vyema. Lakini pia wapo wanaoweza kueleza, furaha haina kipimo - kwamba bila kujali kabichi kuonekana mboga ya "walalahoi," lakini bado inatimiza lengo kuu; shibe.*

*Huo ni uhuru wa kila mmoja kujieleza. Sasa basi, Pambazuko linakupa nafasi ya kuandika maelezo mazuri ya picha hii na kutuma kwa Mhariri kupitia namba hii; 0744 768263. Mwenye maelezo mazuri zaidi, baada ya kupitishwa na wahariri, anaweza kupewa zawadi ya Vocha ya Sh.10,000 kwa mtandao atakaochagua. (Picha hii imechukuliwa kwenye mitandao ya kijamii, haikutambulika mara moja imepigwa wapi na nani).*



GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 0000448.

